JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA**

# TANGAZO KWA UMMA

## UTEKELEZAJI WA UTARATIBU WA UUZAJI, UNUNUZI NA URASIMISHAJI WA BIASHARA YA MAZAO KATIKA WILAYA YA TANGANYIKA MSIMU WA MASOKO 2025/2026.

**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika anapenda kuwatangazia wafanyabiashara wote wa mazao juu ya taratibu za uuzaji na ununuzi wa mazao ya Kilimo kwa Msimu wa masoko wa 2025/2026 ambazo kila Mfanyabiashara anatakiwa kuzifuata kama ifuatavyo:**

1. Kila mfanyabiashara kutoka ndani ya nchi anatakiwa kusajiliwa katika Halmashauri na kupewa kibali maalum cha ununuzi wa mazao katika vituo/maghala au masoko yaliyosajiliwa na kutambuliwa na Halmashauri.
2. Mfanyabiashara yeyote haruhusiwa kwenda kununua mazao moja kwa moja kwa mkulima (shambani/nyumbani) isipokuwa kupitia vituo maalum vilivyosajiliwa.
3. Wafanyabiashara wenye mikataba ya ununuzi wa mazao ya wakulima wanapaswa kuwasilisha nakala za mikataba hiyo Halmashauri.
4. Kuhakikisha kila mmiliki wa ghala au mwendesha ghala anatoa taarifa sahihi za kiasi cha mzigo anachoingiza na anachotoa katika ghala au stoo yake.
5. Ushuru wa mazao utalipwa kwa mujibu wa sheria ndogo za Halmashauri kama ifutavyo;
    - Mahindi Tsh 2,000/= kwa gunia la kilo 100,
    - Mpunga Tsh 2,500/= gunia la kilo 75,
    - Mchele Tsh 3,500 gunia la kilo 100 na
    - Maharage Tsh 3,500 gunia la kilo 100
6. Kabla ya kusafirisha mazao Mfanyabiashara atalipa ushuru kwenye kijiji husika/geti ambalo yupo karani wa mapato na stakabadhi pitapaswa kuonesha yanakopelekwa



Scanned with CamScanner

7. Mfanyabiashara yeyote atakayekamatwa kwa kosa la kutorosha au kufanya vitendo vya kupelekea utoroshaji wa mazao atalipa faini ya kuanzia shilingi laki tatu (300,000) hadi shilingi milioni moja (1,000,000)
8. Mkulima yeyote atakayetoa mazao shambani kwenda nyumbani au kijiji cha jirani anatakiwa kuwa na kibali cha mkulima kutoka ofisi ya kijiji husika
9. Mfanyabiashara yeyote anayesafirisha mazao kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kwenda nje ya Wilaya anatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha mazao kinachotolewa na mtendaji wa Kata/Kijiji/karani wa mapato
10. Mazao yote yanapaswa kuuzwa au kununuliwa kupitia vituo maalum vilivyosajiliwa/kuainishwa na Halmashauri kila kijiji isipokuwa mazao yaliyo chini ya bodi mbalimbali za mazao yakiwemo Tumbaku, Pamba na Ufuta (ambayo yatasimamiwa kwa mujibu wa taratibu za bodi husika).

**Tangazo hili limetolewa na**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
TANGANYIKA

Shabani J. Juma
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA**



Scanned with CamScanner